



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Unapojibu tafadhali taja:-
Kumb. Na: WDC/A.10/11/58

22 Julai, 2022

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa, uwezo na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe kujaza nafasi kama ifuatavyo:-

1. DEREVA DARAJA LA II (Nafasi 4).

a) Sifa za Muombaji:

Awe amehitimu elimu ya Kidato cha Nne (Form IV) na leseni ya Daraja E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Standi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali. Waombaji wenye cheti cha Majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

b) Majukumu ya Kazi.

- Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari,
- Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi,
- Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari,
- Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali,
- Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari
- Kufanya usafi wa gari, na
- Kufanya kazi nyingine kadiri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.

c) Mshahara.

Kwa kuzingatia viwango vya Serikali yaani Mshahara wa **TGS B**

2. MASHARTI YA JUMLA

- Waombaji wote wawe raia wa Tanzania na wenye umri kati ya miaka 18 - 45.

Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, S. L. P. 64 Njombe, Simu/Nukushi Na: +255026 2782111,
Tovuti: www.wangingombcdc.go.tz, Barua pepe:ded@wangingombcdc.go.tz.

- ii. Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa.
- iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V.) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- iv. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vya kidato cha nne na cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
- v. Testimonials, "provisional results", "statement of results", hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita HAVITAKUBALIWA.
- vi. Waombaji waambatishe picha moja ya "Passport size" ya hivi karibuni.
- vii. Barua ya maombi iandikwe kwa mkono.
- viii. Waombaji ambao walisoma nje ya nchi vyeti vyao vya Taaluma vifanyiwe ulinganishi na TCU na NECTA na majibu ya ulinganisho yaambatanishwe kwenye barua ya maombi ya kazi.

Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 05 Agosti, 2022.

Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya: www.wangingombedc.go.tz

MAOMBI YOTE YATUMWE KWA:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe,
S.L.P 64,
NJOMBE.

Imetolewa na:-



Maryam A. Muhaji
MKURUGENZI MTENDAJI (W).
WANGING'OMBE.



**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
WANGING'OMBE**

Jiandae Kuhesabiwa Siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022

Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, S. L. P. 64 Njombe, Simu/Nukushi Na: +255026 2782111,
Tovuti: www.wangingombedc.go.tz, Barua pepe:ded@wangingombedc.go.tz.